**HALMASHAURI YA WILAYA KILINDI**
**SHULE YA SEKONDARI KWEDIBOMA**

**S.L.P 10 SONGE – KILINDI**

Kumb.Na.KWSS/JI/01
MWANAFUNZI …………………………………………………………
SHULE YA MSINGI ……………………………………………………

## YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA……….

Nafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii kuanzia Januari ……….. Ni matumaini yangu kuwa nawe umefurahia vyema nafasi hiyo. Siku za kuripoti shuleni ni kuanzia tarehe……………….,januari mwisho ni tarehe………………..januari.

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:**

**A. SARE ZA SHULE**

*i. Wavulana:*

Shona suruali 2 nyeusi.Nunua shati 2 nyeupe mikono mifupi.Suruali ziwe na mifuko mitatu na zisishonwe kihuni na lazima zivaliwe na mkanda mweusi wenye bekoni ndogo.Tai nyeusi 2,viatu vyeusi jozi mbili (2).

*ii. Wasichana :*

Shona sketi mbili (2) za rangi ya bluu iliyopauka (sky blue).Nunua shati 2 nyeupe mikono mifupi,sketi iwe na marinda nchi moja na nusu na urefu chini ya magoti,tai mbili za rangi ya sketi,soksi pea mbili nyeupe isizo na mapambo,viatu vyeusi vya kamba pea mbili visivyo na visigino virefu,viatu vya bajaji haviruhusiwi.Vazi la hijabu linaruhusiwa na lifanane na sare ya shule.
Angalizo
Nguo ztakzoshonwa tofauti na sare ya shule hazitakubaliwa.

*iii.* Sare ya T-shirt kwa wanafunzi wote inapatikana shuleni kwa gharama ya tsh.8,000/=

**B: VIFAA VYA MADARASANI**

i. Daftari 12 au kaunta 9 za quire 3 (Qr 3)
ii. Mkebe wa mahesabu
iii. Kalamu za kutosha na penseli
iv. Kamusi (dictionary)
v. Begi la kubebea madaftari

**C.VIFAA VYA USAFI**

*WAVULANA*

- Waje na jembe na fagio

*WASICHANA*

- Waje na ndoo na panga

**D: MUHIMU:**

1. Ili uwze kuwasiliana kwa kiingereza itabidi ujifunze kwa bidii
2. Kama mwanafunzi zingatia nidhamu na kujifunza kwa bidii
3. Mzazi uhudhurie vikao vya wazazi ukihitajika.

**E: SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa ***Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978***, Aidha inazingatia miongozo yote inayotlewa na Wizara yenye dhamana ya elimu nchini.Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a. Heshima kwa viongozi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b. Mahudhurio katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
c. Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (preparation)
d. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utazopewa
e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kwa ukamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wowote wa uanafunzi wako katika shule hii
f. Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule
g. Kuvaa sare ya shule wakati wote inapotakiwa
h. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote

**E. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE.**

1. Wizi
2. uasherati na ushoga
3. ubakaji
4. ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, cocaine, mirungi, kubeli, ugoro n.k
5. kupigana au kupiga
6. kuharibu kwa makusudi mali ya umma
7. kudharau bendera ya taifa
8. kuoa au kuolewa
9. kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
10. kutoa mimba
11. kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
12. Kukataa adhabu kwa makusudi
13. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi haruhusiwi.

**F. MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI**

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kutatekeleza kikamilifu.

a. Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni
b. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai
c. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakotolewa na shule
d. Lete nakala ya cheti cha kuzaliwa (birth certificate) au kama huna lete hati ya kiapo kutoka mahakamani (AFFIDAVITY)

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

Daniel
..............................

ENNEDY DANIEL

0752-025674

MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI
KWEDIBOMA

# MEDICAL CERTIFICATE FORM

To be completed by medical officer in respect of FORM ONE entrant.

Pupils full name ……………………………………………………………………

Age ……………………………………………………………………………

Blood count (red and white) ……………………………………………………

Stool examination ……………………………………………………………

Urinalysis ………………………………………………………………………

Pregnancy ………………………………………………………………………

Syphilis test ……………………………………………………………………

T. B test ………………………………………………………………………

eye test ………………………………………………………………………

ears ……………………………………………………………………………

chest ……………………………………………………………………………

spleen …………………………………………………………………………

Abdomen ………………………………………………………………………

**ADDITIONAL INFORMATION**: e.g. Physical defect or impairments, infections, chronic or family diseases e.t.c

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

I certify that the above is fit/unfit for admission into a day/boarding secondary school.

Signature ………………………………………………………………………

Designation ……………………………………………………………………

Station …………………………………………………………………………

Date ……………………………………………………………………………

# SHULE YA SEKONDARI KWEDIBOMA

## UTHIBITISHO WA KUKUBALI KUJIUNGA

Jina la Mzazi / Mlezi ..........................................................................................
Mimi mzazi / Mlezi wa ...................................................................................
nakubali kuchukuwa nafasi aliyopewa mtoto wangu kujiunga na kidato cha kwanza mwaka .................... Ninaahidi kuwa nitafuatilia mwenendo wa mtoto wangu na kumsaidia katika masomo yake nikishirikiana na walimu. Aidha nitahakikisha kuwa mtoto wangu anahudhuria na anafuata sheria za shule na taratibu zote.

Sahihi ya mzazi/Mlezi .............................................. Tarehe ..................................

## UTHIBITISHO WA MWANAFUNZI

Mimi ...................................................... nakubali kuchukua nafasi niliyopewa kidato cha kwanza. Ninakubali nafasi hii kwa matakwa yangu na ninaahidi kusoma kwa bidii na kufuata SHERIA na MASHARTI yote ya shule.

Sahihi ya mwanafunzi ............................................. Tarehe .......................................